Makete DC Habari
Karibu uwekeze Makete
Octoba 2022

# Wanufaika wa TASAF Mfumbi wajivunia ufugaji wa mbuzi



*Bi. Tovonisye Msite mnufaika wa mpango wa kunusuru kaya Maskini (TASAF) mkazi wa Kijiji cha Ikovo akiwa machungoni.*

Wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya Maskini unaotekelezwa na mfuko wa maendeleo Jamii (TASAF) Kijiji cha Ikovo Kata ya Mfumbi Wilaya ya Makete Mkoani Njombe wameishukuru Serikali kwa kubadilisha maisha yao kupitia ufugaji.

Shukrani hizo zimetolewa wakati Afisa usimamizi wa TASAF Wilaya ya Makete Bw. Hery Mpunza alipokuwa katika ufuatiliaji wa miradi na kuangalia namna ambavyo wanufaika wa miradi ya TASAF wanavyoendesha shughuli zao za ufugaji.

Kaya ya Bi. Tovonisye Msite ni moja ya kaya zinazonufaika na mpango huo wa TASAF. Tuvonisye ni mjane na kaya yake inawatoto wawili ambao kwa sasa wanasoma kati ya hao mmoja anasoma shule ya Sekondari Mt. Chafukwe na mwingine shule ya Msingi Ikovo.

Mjane huyo alipokea Mbuzi 6 mwaka 2020 na wamezaliana hadi kufikia mbuzi 18 hadi sasa.

Mjane huyo amekuwa akiuza mbuzi amefanikiwa kuwasomesha wajukuu wake kwa kuwanunulia mahitaji ya shule pamoja na mahitaji mengine ya msingi. Pamoja na kulea watoto amefanikiwa kuanza ujenzi wa nyumba yenye vyumba vitatu.



*Bi. Tovonisye Msite akiwa kwenye makazi yake, kushoto ni nyumba mpya anayoijenga kupitia ufugaji wa mbuzi aliowezeshwa na TASAF.*

Pia Bi. Tuvonisye kupitia mradi huo amefanikiwa kukodi mashamba yenye ukubwa wa ekari 2.5 kwa ajili ya Kilimo cha mahindi kwa msimu wa mvua unaokaribia kuanza mwezi Novemba, 2022.

"Mashamba haya yatanisaidia kuzalisha mahindi ambayo yatanipatia chakula lakini pia naweza kuuza ni nikapata fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali haikuwa rahisi kufikia hapa nilipo naishukuru sana TASAF kwa kunisaidia" Alisema Bi. Tuvonisye.



***Baadhi ya wanufaika wa TASAF ambao wamekusanya mifugo (Mbuzi) na kupeleka malishoni karibu na makazi yao Kijiji cha Ikovo (Wote ni wanufaika wa mpango wa kunusuru Kaya Maskini TASAF)***

Kaya ya Elizabeth Mbilinyi ni mojawapo ya wanufaika wa TASAF ambao imewasaidia kubadilisha maisha kwa kuingiza umeme kwenye nyumba, kujenga choo cha kisasa na kuongeza ufugaji wa kuku.

"Kwa sasa nimeboresha mazingira ya familia hapa nyumbani tunaishi kwenye nyumba yenye umeme hatulali giza tena, lakini hata chooni kumekuwa na mazingira rafiki tofauti na hapo awali".

"Nikiwa na uhitaji wa fedha kwa sasa nauza mbuzi muda wowote inanisaidia kutatua matatizo mbalimbali ya kifamilia kwa wakati...kwa kweli nimeondoka katika hali ya mawazo na sasa najisikia faraja muda mwingi". Aliongeza Elizabeth Mbilinyi



***Elizabeth Mbilinyi mnufaika wa TASAF kijiji cha Ikovo Kata ya Mfumbi Wilayani Makete akijiandaa kupeleka mifugo malishoni.***

Angombwise Kilongo mwenye umri zaidi ya miaka 70 ni mnufaika wa mpango huo ambaye alipata mbuzi 6 kutoka TASAF amefanikiwa kuwafuga na baada ya kuzaliana wamefikia 20.



*Kushoto ni Hery Mpunza Afisa ufuatiliaji TASAF Wilaya ya Makete akizungumza jambo na mmoja wa wanufaika wa TASAF Bi. Angombwise Kilongo nyumbani kwake Kijiji cha Ikovo.*

Amesema mpango huo umemsaidia kupeleka wajuu wake shuleni ambapo mmoja amehitimu kidato cha nne 2021 na mwingine akiendelea na masomo shule ya Msingi Ikovo.

Bi. Angombwisye anasema amefanikiwa kuingiza umeme kwenye nyumba yake mara baada ya kuuza mbuzi 9 na kujenga choo cha kisasa huku akihakikisha mwanafunzi hakosi chakula awapo shuleni na mahitaji mengine muhimu.

“Mimi ni mnufaika wa TASAF nilifanikiwa kufuga mbuzi na baada ya kuzaliana nikapata faida nikauza baadhi ya mbuzi na kuanza ufugaji wa kuku ambapo nilianza na kuku watano (5) na sasa nina kuku nane na wameanza kutaga mayai ambayo anauza na kula” Ameongeza Bi. Angombwisye.

Nehemia Sanga ni mnufaika wa mpango huo akiwa hana wazazi alikuwa akilelewa na mama wa kambo pamoja na mdogo wake ameishukuru Serikali kwa kumsaidia kumpatia mbuzi ambazo amesema baada ya kuzaliana zimemsaidia kujenga nyumba, kuoa na sasa anafamilia ya watoto wawili.

Sanga anasema pamoja na ufugaji huo wa Mbuzi bado anaendelea kufanya ufugaji wa kuku wa kienyeji huku akiendelea kufanya vibarua vya kulima mashamba ya watu ili kujiongezea kipato.



*Bw. Nehemia Sanga akiwa kwenye banda la Mbuzi nje ya nyumba yake, pia amesema amefanikiwa kukusanya mbolea ya mifugo ambayo inamsaidia katika uzalishaji wa mazao na kumpounguzia gharama za kununua mbolea ya Viwandani*



***Kushoto ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Ikovo Bw. Kornelio Mwata akiwa ameongozana na Hery Mpunza Afisa ufuatiliaji wa TASAF (W) Makete pamoja na baadhi ya wanufaika wa mpango wa kunusuru Kaya Maskini wakati walipokuwa wakiwatembelea kukagua miradi yao inavyoendeshwa sambamba na mifugo***



Huyu ni moja ya wanufaika wa TASAF kijiji cha Ikovo Bw. Silaka Sanga akimpatia pumba mbuzi wake.



***Baadhi ya Mbuzi wa wanufaika wa TASAF Kijiji cha Ikovo wakiwa wamehifadhiwa kwenye banda baada ya kutoka kwenye malisho.***

# Watendaji Kata wasaini Mkataba kusimamia Lishe

Watendaji wa Kata zote 23 Wilayani Makete wamesaini Mkataba wa lishe ngazi ya Jamii katika Kata zao mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Makete Mhe. Juma Sweda.

Mkataba huo ulisainiwa 24 octoba 2022 katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Makete kwa lengo la kupambana na Utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano (5).

Mkuu wa Wilaya ya Makete Mhe. Juma Sweda amewaagiza watendaji wa Kata kuhakikisha wanasimamia shughuli za Lishe kwa watoto kwenye Kata zao ili kuwa na watoto wenye Afya bora kwa kuwa Wilaya ya Makete inazalisha mazao ya aina mbalimbali ambayo yanaweza kusaidia kupambana kwa kiasi kikubwa katika kuepuka utapiamlo kwa watoto.



*Afisa Utumishi Humphrey Mushi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji (W) William M. Makufwe akisaini Mikataba ya lishe na watendaji wa Kata, zoezi lililofanyika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Makete*

Akizungumzia hali ya Utapiamlo katika Wilaya ya Makete kwa kipindi cha Julai-Septemba 2022, Afisa Lishe Wilaya Bi. Jakline Nannauka amesema hali ya Lishe ni nzuri kwa 98% na elimu kwa wananchi inaendelea kutolewa kuhusu umuhimu wa lishe bora kwa watoto ili kufikia lengo la 100%.

"Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, hali ya lishe katika Wilaya ya Makete kwa kipindi cha Julai-Septemba ni nzuri kwa 98%, na wazazi na walezi wanaendelea kupata elimu kutoka kwa wahudumu wetu wa Afya kwa kutoa elimu kupitia kaya kwa kaya na kuhakisha wananchi wote wanafikiwa na elimu kuhusu lishe hususan wanawake wajawazito".

Mganga Mkuu Wilaya ya Makete Ligobert Kalisa amesema Wilaya ya Makete inaongoza kwa kuwa na lishe bora kwa watoto katika Mkoa wa Njombe na kushika nafasi ya 16 Kitaifa jambo ambalo linaashiria hali ya lishe kuwa bora.

"Wilaya ya Makete imekuwa ya kwanza kimkoa na imeshika nafasi ya 16 Kitaifa katika suala la lishe hivyo hatuna budi kuwapongeza Viongozi na wananchi, na matarajio yetu Octoba-Disemba, 2022 tuwe katika nafasi nzuri zaidi Kitaifa"

Kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, Afisa Utumishi na raslimali watu Bw. Humphrey Mushi akisaini mikataba hiyo na watendaji wa Kata amewasihi kuwajibika kwa upande wao kama watumishi kuhakikisha wanatekeleza ipasavyo majukumu yao ili kuwa na Jamii yenye Afya imara.

"Niwasihi tu watumishi wenzangu watendaji wa Kata, Mikataba hii siyo iishie kwenye makaratasi tu bali ni katika uhalisia wa utendaji wetu na hiki ni kipimo cha uwajibikaji kwetu…hivyo tukafanye kazi ya kuhamasisha wananchi wapate elimu kuhusu lishe mkishirikiana na wataalamu wa Afya na wahudumu wa Afya ya Msingi ngazi za vijiji"

Kwa upande wake Mtendaji Kata ya Ikuwo Mtunyule Joachim amesema wao kama viongozi wasimamizi ngazi ya Kata watahakikisha hali ya lishe inaboreshwa zaidi katika Kata zao kwa kuongeza uwajibikaji kwa Mzazi au mlezi mwenye mtoto chini ya miaka mitano.

"Ndugu zangu watendaji kwa umoja wetu najua tulivyosaini hapa sasa ni kwenda kuhakikisha tunawafikia wananchi wetu kila mwenye mtoto chini ya miaka mitano kumpa elimu ili asipatikane mtoto mwenye utapiamlo au lishe duni kwenye kata zetu…nikuhakikishie Mkuu wa Wilaya Makete inakwenda kuwa ya kijani kila kona".

# Bilioni 9 kutatua kero ya Maji Makete

Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Antony Sanga amesema miradi ya maji yenye thamani zaidi ya shilingi Bilioni 9 inatekelezwa katika kipindi cha mwaka 2022/23.

Akizungumza kwenye uwekaji wa jiwe la Msingi mradi wa maji Kata ya Mbalache utakaohudumia vijiji viwili ambavyo ni Lupombwe na Mbalache mradi unaojengwa kwa ufadhili wa Jumuiya ya Kanisa la Kilutheri ya Hamburg Blankenese Ujerumani kwa kushirikiana na Serikali, Mhandisi Sanga amesema Serikali imepanga kufikia 2025 wananchi wa vijijini wawe wanapata maji kwa 85% hivyo Wilaya ya Makete inatekeleza miradi mbalimbali ili kusogeza huduma ya maji karibu na wananchi.



*Mhandisi Antony Sanga akizungumza na wananchi wa Kata ya Mbalache mara baada ya kukamilika kwa zoezi la uwekaji jiwe la Msingi mradi wa Maji Mbalache*

Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha za kutekeleza miradi ya maji yenye zaidi ya Bilioni tisa (9) katika Wilaya ya Makete kwa lengo la kumtua mama ndoo kichwani na kupata huduma karibu na maeneo wanayoishi wananchi.

"Serikali sikivu ya Mama Samia Suluhu Hassan imejipanga kuhakikisha changamoto ya maji vijijini inapungua kwa 85% ambapo tayari Mheshimiwa Rais amekwishatoa fedha za kujenga miradi katika maeneo mbalimbali Wilayani hapa".



*Baba Askofu William Sanga akiweka jiwe la Msingi ujenzi wa Mradi wa Maji Mbatche*

# Wananchi zaidi ya elfu 2,000 kunufaika na mradi wa Maji Mbalache

Pia Katibu Mkuu huyo akizungumza na wanamakete waliohudhuria katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi mradi wa maji amewasihi kutunza vyanzo vya maji na mazingira ili kuendelea kuwa na uhakika wa maji kwa kipindi chote cha mwaka, huku akiwasihi kutunza na kulinda miundombinu ya maji wakati wote.

Baba Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania-Dayosisi ya Kusini Kati (KKKT-DKK Makete) Mch. William Sanga amesema Kanisa limeendelea kutimiza wajibu wake wa Kitume kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo kusogeza huduma ya maji karibu zaidi na Wananchi.

"Sisi kama Kanisa pamoja na kuwalea wananchi kiroho lakini jukumu letu kubwa pia ni kuhakikisha tunashiriki kikamilifu kuwapatia wananchi huduma muhimu ikiwemo Afya, Elimu, Maji na vitu vingine…kwa hiyo hili ni jukumu letu kubwa kuungana na Serikali kuwasaidia wananchi wetu".

Mchungaji Klaus Poehls Mwakilishi wa Kanisa la Kilutheri Hamburg Blankenese Ujerumani amesema mradi huo utafanya kazi ya kuhudumia wananchi wa Mbalache na Lupombwe huku akiwapongeza kwa bidii waliyoitoa wakati wote wa ujenzi wa Mradi huo

Mkurugenzi Mtedaji Halmashauri ya Wilaya ya Makete William Makufwe amewashukuru wanajumuiya hao kwa kuisaidia Serikali kufikisha huduma kwa wananchi huku akiwataka wananchi wa Mbalache kuutunza mradi huo na kulinda mazingira

"Tunawashukuru sana wanajumuiya kutoka ujerumani kwa kushirikiana na Kanisa kwa ujenzi wa mradi huu mkubwa…mmeisaidia Serikali kuwapunguzia wananchi adha ya maji kwa muda mrefu na sasa huduma imesogea karibu kabisa na makazi yao".

Mkurugenzi wa Udiakonia Elikana Kitahenga amesema mpaka kukamilika kwa mradi huo utakuwa umegharimu kiasi cha shilingi Bilioni 1 na milioni 200 huku ukitarajia kuhudumia wananchi zaidi ya 2000

Kwa upande wao wananchi wa Mbalache wamewashukuru wadau hao na Serikali kwa kuwapelekea mradi huo mkubwa wa maji ambao unakwenda kutatua changamoto ya uhaba wa maji katika vijiji vyao.






***Imeelezwa kuwa mradi huu wa maji utasaidia wananchi wa Kijiji cha Mbalache na Lupombwe kuondokana na adha ya maji kwa muda mrefu, Pia Wanafunzi shule ya Sekondari Mbalatse watanufaika na mradi huo sambamba na Kituo cha Afya kinachojengwa na Halmashauri kwa shilingi Milioni 400 kwa kutumia mapato ya ndani.***

# Madiwani Makete wapongeza Watendaji kwa kuibua miradi ya Maendeleo



***Mwonekano wa Bwalo linalojengwa shule ya Sekondari Mang'oto ambalo litatumika kwa ajili ya chakula, mikutano, Mitihani, Mahafali pamoja na shughuli mbalimbali za mikusanyiko.***

Serikali kupitia TASAF inajenga bwalo kubwa shule ya Sekondari Mang'oto iliyopo Kata ya Mang'oto kwa gharama ya zaidi ya Milioni 192 ikiwa mchango wa Serikali kupitia TASAF ni Milioni 170 na nguvu za wananchi ni 18% sawa na shilingi Milioni 22.

Mradi huo unatekelezwa kwa Milioni 192 na wananchi kutoka vijiji viwili ambavyo viliibua mradi huo wanasaidia nguvu kazi kuhakikisha mradi huo unakamilika .

Kazi hiyo ilianza mwezi wa nne 2022, wakati wa utekelezaji wa mradi zilijitokeza changamoto mbalimbali ikiwemo wananchi kupunguza nguvu kazi.

Diwani Kata ya Mlondwe Mheshimiwa Alphonse Salimo ambaye ni mjumbe wa Kamati ya Fedha mipango na Utawala aliwapongeza wasimamizi wa mradi huo kwa usimamizi wa karibu kuhakikisha mradi unatekelezwa kwa kiwango kinachostahili.

Mheshimiwa Diwani Kata ya Lupila Ernesta Lwilla aliwapongeza wananchi wa Kata ya Mang'oto kwa ushirikiano wanaouonesha katika utekelezaji wa mradi huo huku akiwasihi kuendelea kushikamana katika kuhakikisha jengo hilo linakamilika kama ilivyopangwa.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Makete Bw. Henry Nyigu akizungumza mbele ya Kamati ya fedha, Mipango na Utawala ilipotembelea kukagua mradi huo Kata ya Mang'oto alisema Serikali imetoa fedha hizo kusaidia wananchi ili kuwapunguzia michango ya ujenzi huo.



***Mkurugenzi Mtendaji (W) William Makufwe kushoto akiwa na baadhi ya wakuu wa Idara eneo la mradi***

# DC Sweda aonya ucheleweshwaji ujenzi Kituo cha Afya Mbalache

Mkuu wa Wilaya ya Makete Mhe. Juma Sweda ameiagiza Kamati ya ujenzi Kituo cha Afya Mbalache kuhakikisha inanunua vifaa vyote muhimu zikiwemo nondo ili kutokwamisha ujenzi wa Kituo cha Afya.

Ametoa agizo hilo akiwa eneo la ujenzi wa Kituo cha Afya Mbalache kukagua na kuona hali ya ujenzi imefikia hatua ipi tangu Serikali ilipotoa fedha miezi miwili iliyopita.

Mheshimiwa Sweda amesema kutokuwepo kwa vifaa katika eneo la ujenzi kunasababisha kuchelewa kwa ujenzi, hivyo ameitaka kamati ya ujenzi kuhakikisha inanunua vifaa vyote ili kuendana na kasi ya ujenzi kwa mujibu wa mkataba.



*Kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Makete Mhe. Juma Sweda akizungumza na Diwani Kata ya Mbalache pamoja na baadhi ya wanakamati waliofika eneo ambalo Kituo cha Afya kinajengwa*

"Hapa hakuna nondo kwa mujibu wa fundi, mnakaa wiki nzima bila vifaa hamuoni kama mnachelewesha kazi? Nataka kesho vifaa vyote ambavyo havipo zikiwemo nondo ziwepo hapa ili fundi aendelee na kazi kwa kasi maana mvua nayo imeshaanza kunyesha niwasisitize kamati acheni uzembe".

Kwa upande wao wananchi waliofika kufanya shughuli ya upangaji tanuri la tofali ili kuzichoma, wameishukuru Serikali kwa kuwapatia fedha za ujenzi wa Kituo hicho na wamesema wapo tayari kuendelea kutoa ushirikiano katika ujenzi huo

"Tunaishukuru Serikali kwa kutupatia fedha, tumeteseka kwa muda mrefu kufuata huduma Ikonda au Wilaya ya Wanging'ombe Kituo cha Afya Kipengere au tufuate huduma Lupila jambo ambalo wanawake wanapohitaji kujifungua wanapata changamoto kubwa ya gharama ya kusafiri umbali mrefu ili kupata huduma".

Halmashauri kupitia mapato yake ya ndani imetoa fedha kiasi cha shilingi Milioni 400 kujenga Kituo cha afya Mbalache kwa lengo la kusogeza karibu huduma kwa wananchi wa Kata hiyo yenye vijiji vitatu ambavyo ni Lupombwe, Mbalatse na Kisasatu



***Wananchi wa Kijiji cha Lupombwe wakishirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Makete Mhe. Juma Sweda wakipanga Tanuru kwa ajili ya kuchoma tofali za kujengea Kituo cha Afya Mbalache.***

# Halmashauri Makete yanunua mashine ya kutengeneza Tofali kwa Mil. 41 ili kusogeza huduma kwa wananchi

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri (W) Makete William Makufwe amesema Halmashauri imenunua mashine ya kutengeneza tofali zaidi ya elfu nne (4,000) kwa siku moja na kutoa ajira kwa vijana.

Tofali hizo zitatengenezwa kwa kutumia mchanga na Saruji kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa miradi ya Serikali ikiwemo Zahanati, Vituo vya Afya, nyumba za watumishi, Madarasa lakini pia zitauzwa kwa wananchi kwa bei ndogo.

Makufwe alisema mashine hiyo imenunuliwa kwa shilingi Milioni 41 na mwishoni mwa mwezi Octoba 2022 itaanza kufanya kazi.

Pamoja na hayo Bw. Emily Maganga ambaye ni Mhandisi wa Halmashauri ameeleza kuwa mashine hiyo imenunuliwa kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa tofali kwa wanamakete ambao walikuwa wakifuata tofali hizo kwa zaidi ya Kilomita 100 kutoka Makambako au Mbeya kwa gharama kubwa ya shilingi 2,000 au zaidi tofali moja pamoja na gharama za usafirishaji hivyo kufanya utekelezaji wa miradi mbalimbali pamoja na ujenzi wa nyumba binafsi kuwa na gharama kubwa.



# Mil. 200 zimekopeshwa kwa Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu Makete

Zaidi ya shilingi Milioni 200 zimekopeshwa na Halmashauri kutoka 10% bila riba kwenye vikundi mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kufanya shughuli za ujasiriamali.

Vikundi hivyo ni vile vinavyojihusisha na Kilimo cha Viazi, ngano, mahindi, Bodaboda, Kilimo cha Miti, uchomaji mkaa na ufugaji wa nyuki.



*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Makete William M. Makufwe*

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Makete William M. Makufwe amesema fedha hizo ni katika kipindi cha robo mwaka kuanzia Mwezi wa 7 mpaka mwezi wa 9, 2022.
Ameongeza kuwa vikundi tisa vya vijana, wanawake vikundi vinne na watu wenye ulemavu wameshanufaika na fedha hizo za 10% kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao za ujasiriamali.

# Mil. 240 kujenga madarasa 12 Makete



*Moja ya Darasa linaloendelea kujengwa kwa fedha za Pochi la Mama katika shule ya Sekondari Usililo Kata ya Luwumbu*

Milioni 240 zimetolewa kupitia Pochi la Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kujenga madarasa 12 katika shule 8 za Sekondari Wilayani Makete

Tayari ujenzi wa Madarasa umeanza katika baadhi ya shule ikiwemo shule ya Sekondari Lupalilo iliyopo Kata ya Tandala ambapo viongozi wa Kata hiyo wamepongeza kwa kuanza mapema ujenzi huo kuliko ilivyotarajiwa

Timu ya Menejimenti ya Wilaya ya Makete ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya William M. Makufwe ilitoa pongezi hizo ikiwa katika shughuli ya ukaguzi wa miradi inayotekelezwa katika kata mbalimbali Wilayani hapa.

Timu hiyo imeagiza mpaka kufikia tarehe 25 Novemba ujenzi wa Madarasa hayo uwe umekamilika kwa matumizi

# Wadau wa Maendeleo Lupila wachangia Mil. 20 kukarabati miundombinu Lupila Sekondari




Wadau wa Maendeleo Kata ya Lupila wamechangia zaidi ya shilingi Milioni 20 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule ya Sekondari Lupila pamoja na kutoa zawadi kama motisha kwa walimu

Wadau hao wanaoishi ndani ya Kata ya Lupila na nje ya Kata hiyo wamekuwa na utaratibu wa kuchangishana fedha ili kuboresha miundombinu ya shule ikiwemo kukarabati madarasa, Bweni, ununuzi wa vitanda na hata kutoa zawadi mbalimbali kwa walimu na wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo yao.



***Wahitimu kidato cha nne Lupila Sekondari wakiimba wimbo wa kuwaaga wadogo zao ukiwa na ujumbe wa kuwatakia masomo mema.***

Akiwa kwenye Mahafali ya Kidato cha nne Mgeni rasmi ambaye pia ni Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Anthony Sanga ambaye pia ni Mhasibu wa umoja wa wadau hao ameshukuru wadau hao kwa kuendelea kuwa na moyo wa kujitolea ili kuboresha miundombinu ya shule hiyo na wanafunzi kujisomea kwenye mazingira rafiki.

Pia Mhandisi Sanga amewapongeza wahitimu kwa uvumilivu wao kwa kipindi chote cha miaka mine na kuwasihi wajiandae vyema kuelekea mitihani yao ya mwisho.

"Sisi kama wadau wa maendeleo katika shule ya Sekondari Lupila tunawapongeza kwa kufanikisha kufikia

# Wahitimu Mkawe raia wema huko Mtaani-Mhandisi Sanga



hapa leo haikuwa kazi rahisi, maana wenzenu baadhi hawajafanikiwa kuhitimu kwa sababu mbalimbali ikiwemo utoro"

"Kwa hiyo wadau tutaendelea kuweka mazingira rafiki ya shule yetu ili wanafunzi msome bila kuwaza kutoroka na kuacha masomo, wadau wa maendeleo Kata ya Lupila tumeshachangia Milioni 20.8 kwa ajili ya kuboresha mazingira ya shule ya shule yetu".

Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Antony Sanga amewasihi wanafunzi Kidato cha nne kufanya vizuri mitihani yao ya kuhitimu na kwenda uraiani kuwa raia wema, wenye nidhamu na kusaidia wazazi majukumu mbalimbali.

Pia Mhandisi Sanga amewapongeza wadau wa maendeleo Kata ya Lupila kwa michango yao katika kuisaidia Serikali kuboresha mazingira ya Shule ya Sekondari Lupila
Ameyasema hayo octoba 15,2022 akiwa kwenye mahafali ya Kidato cha nne shule ya Sekondari Lupila iliyopo Kata ya Lupila Wilayani Makete Mkoani Njombe



***Wahitimu Kidato cha sita 2022 waliofanya vizuri kwenye matokeo wakiwa katika picha na mgeni rasmi mara baada ya kukabidhiwa zawadi kutoka kwa wadau wa Maendeleo Kata ya Lupila.***

***Kwa matokeo ya Kidato cha sita shule ya Sekondari Lupila imeshika nafasi ya kwanza Katika mkoa wa Njombe, ikumbukwe hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwa wahitimu hao kufanya mtihani kwa shule hiyo tangu ilipoanzisha Masomo ya Kidato cha tano miaka miwili iliyopita.***